

BWANA TUNAANGAMIA

Na, Deogratius Dotto

SUA-Morogoro.

20 August 2019.

KWA HISIA

1. U li mwe ngu ni ni li mo ni ma te so, na ma ha nga i ko ya ha pa na pa le,

Mo yo wa ngu wa u mi a nda ni ya ngu, ho fu na te te me ko li me ni

9

ji a, Te ge me o la ngu ndi we Ye su wa - ngu.

16

ji a, Te ge me o la ngu ndi we Ye su wa - ngu.

2. Magonjwa ya kutisha yametawala, Ebora, UKIMWI vya maliza watu, Wakubwa na wadogo waangamia, sikitiko kuu kwa ndugu jamaa, Wapokee wapokee Bwana wangu.
3. Vita vya kikatiri navyo vyatanda, watu wengi kweli wauana ovyo, Na janga la njaa nalo la ukame, chakula kimekuwa tatizo kubwa, Tuokoe tuokoe Bwana wangu.
4. Ona ajali ile ya Morogoro, watu walivyoteketea kwa moto, Wenye hatia na wasio hatia, wote kwa pamoja waliteketea, Wapokee wapokee Bwana wangu.
5. Dhoruba kali pia nayo tufani, vimepoteza watu wengi majini, Kwa ajali ya meli ya Zanzibar, pia na kivuko cha Feri cha Mwanza, Vimeangamiza watu wengi sana.
6. Vyombo vya angani ndege zadondoka, zidondokapo hakuna masalia, Kila kitu kweli chaishia hapo, ni majivu tupu ndiyo ushahidi, Tunaangamia Bwana tuokoe.
7. Nafsi yangu yakungojea Mwokozi, utaporudi kuja kunichukua, Nikaishi nawe Mbinguni kwa Baba, Kwenye makao yaliyo ya milele, Nitafu milele hata milele.